Ushauri kwa wakimbizi walio Wasagaji, Wasenge, Huntha na wa jinsia mbili (LGBT) nchini USkoti

Aprili 2011

LGBT - Swahili

Tunathamini utofauti na hutendea watu wote sawa na kwa hadhi na heshima.

Kwa bahati mbaya, watu wengine hupitia udhalilishaji na/au ushambulizi kwa sababu ya hali yao ya kijinsia au jinsia wanayojitambulisha nayo (utambulisho wa jinsia). Iwapo umepitia dhuluma, ushambulizi au kuteswa kwa sababu wewe ni msagaji, msenge au huntha (LGBT) na ungependa kudai kimbilio katika Uingereza, kijitabu hiki hutoa maelezo kuhusu mahali ambapo unaweza kupata usaidizi, ushauri na maelezo.

Makubaliano ya Wakimbizi ya 1951 yanasema:

> *"mtu yeyote ambaye – kwa sababu ya woga wowote wenye sababu wa kuteswa kwa sababu ya rangi,dini, uraia, uanachama wa kikundi chochote au mtazamo wa kisiasa na yuko nje ya nchi yake asili, na hawezi kwa sababu ya woga huo, kujisalimisha kupata ulinzi katika nchi hiyo"*

Mpaka hivi karibuni ilikuwa vigumu kwa msagaji, msenge, au huntha (LGBT) kuthibitisha kuwa walifikia kiwango kilicho hapo juula kudai utafutaji kimbilio katika Uingereza. Mnamo Julai 7 2010, Uamuzi wa Mahakama Kuu kati ya – *HJ (Iran) na HT (Cameroon) dhidi ya Ofisi ya Katibu Mkuu wa Idara ya Nyumbani [2010 UKSC 31]* – ilionyesha kuwa iwapo watu walikuwa wakiteswa kwa sababu ya ya hali mtazamo wao wa kijinsia, basi wanapaswa kulindwa na Ofisi ya Nyumbani. Uamuzi huu haulindi moja kwa moja kesi za huntha lakini unaweza kuwa muhimu. Maelezo kamili kuhusu uamuzi huu unapatikana kwenye tovuti ya Mahakama Kuu ya Uingereza:

http://www.supremecourt.gov.uk/docs/UKSC_2009_0054_Judgment.pdf

amuzi huu wa Mahakama Kuu unamaanisha nini kwa Wasagaji, Wasenge au Huntha (LGBT) ?

Iwapo unatafuta ulinzi kwa sababu ya hali yako ya kijinsia au jinsia unayotambulisha (utambulisho wa kijinsia), kuna usaidizi zaidi wa kisheria unaoweza kukusaidia. Ni muhimu kukumbuka kuwa hata ingawa kuna vizuizi katika kutuma ombi la utafutaji kimbilio na vimeondolewa, hutapewa kimbilio katika Uingereza.

Korti iliamua kuwa watafutaji kimbilio walio wasagaji au wasenge hawatarajiwi kujilinda kutokana na kuteswa katika nchi yao asili kwa kuficha hali yao ya kijinsia. Uamuzi huu huongeza uzito kwa Ofisi ya Nyumbani kubishana kuwa utakuwa salama iwapo utakwenda kwa nchi yako ya asili kwa kuficha kuwa wewe ni msagaji, msenge au huntha.

Makubaliano ya sasa ya Serikali ya Uingereza uliotolewa mnamo Mei 20, 2010 ni pamoja na taarifa ifuatayo:
“Hatutasitisha urudishaji nyumbani wa watafutaji kimbilio ambao wametoka kwa nchi tofauti kwa sababu jinsia yao au utambulisho wao wa kijinsia huwaweka katika hatari ya kukamatwa, kuteswa au kuuliwa.”

Ninapaswa kufanya nini iwapo mimi ni mssagaji, msenge, huntha (LGBT) na nimeteswa katika nchi yangu kwa sababu ya hali yangu ya jinsia au utambulisho wangu wa jinsia?

Iwapo umepitia mateso kwa sababu ya tabia au utambulisho wako wa kijinsia, unapaswa ku:

- Eleza Ofisi ya Nyumbani katika **nafasi ya kwanza utakayopata.** Iwapo jambo hili linaweza kuwa gumu, usipowaeleza, kustahilika kwako kunaweza kuwa na athari mbaya kwa mafanikio ya utafutaji wako wa kimbilio.
- Shirika hiii na mshauri unayemwamini, kama vile mmoja wa wafanyakazi wetu, mshauri katika shirika lingine la wakimbizi au mwakilishi wako wa kisheria. Mshauri wako yupo hapo kusaidia na kila unachomweleza huwekwa kwa usiri. Wataweza pia kutambua wataalamu wengine ambao wanaweza kukusaidia.
- Pata au chagua mwakilishi wa kisheria anayeelewa kuhusu kesi za usagaji, usenge au uhuntha (LGBT). Iwapo hawana uzoefu katika eneo hili, hakikisha kuwa wanaelewa kuhusu kesi kama ilivyoonyeshwa hapo juu.

Ni nani anaweza kunisaidia?

Mawakala wa wakimbizi na vikundi vya vipindi vya hiari

Mawakala wa wakimbizi, kama Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti, na vikundi vingine vya hiari- pamoja na mashirika ya wasagaji, wasenge au huntha (LGBT)– wanaweza kukusaidia kupata maelezo na usaidizi unaohitaji. Hii inaweza kuwa kukusaidia kufikia vikundi vya kisheria, afya au jamii. Wanaweza pia kukusaidia iwapo unapitia dhuluma, kwa mfano,katika makao yako au makazi.

Mawakala hawa watahesgimu usiri wako na hawatajadiliana tondoti zako na mtu yoyote ila uwaruhusu kufanya hivyo. Ufaragha pia unahusika na wakalimani; lazima wawe na tabia za utaalamu na wala sio kujadiliana maelezo yakona mtu yeyote.

Unaweza pia kutoa ombi la kutafsiri kwenye simu iwapo unahisi starehe ukongea na mtu kwenye simu.

Orodha nyingine ya tovuti muhimu ni :

Equality Network

www.equality-network.org/Equality/website.nsf/home?OpenForm

LGBT Youth Scotland

www.lgbtyouth.org.uk

Stonewall Scotland

www.stonewall.org.uk/scotland

Scottish Transgender Alliance

http://www.scottishtrans.org/

UK Lesbian and Gay Immigration Group

32-36 Loman Street, London, SE1 0EH
Simu: 0207 922 7811
http://www.uklgig.org.uk/asylum.htm

Kuripoti ushambulizi

Polisi huwasaidia sana wasagaj, wasenge na huntha (LGBT). Unaweza kuwasiliana na Ofisaa wao wa Uhusiano wa LGBT.

Iwapo huwezi au hutaki kuzungumza moja kwa moja na polisi, unaweza kutumia njia ya usiri ya kuripoti ya mtu wa tatu. Hili hukuruhusu kuripoti ushambulizi kwa mfanyakazi katika wakala kala Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti (0800 085 6087). Mtu huyo atachukua tondoti utakazotoa na unaweza kuchagua iwapo ungependa polisi wachunguze.